



## Hawezi kuwa na imani mmoja wenu mpaka ampendeleee ndugu yake anachokipenda yeye katika nafsi yake

Kutoka kwa Abuu Hamza Anas bin Maaliki radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake mtumishi wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake amesema: "Hawezi kuwa na imani mmoja wenu mpaka apendeleee ndugu yake anachokipenda yeye katika nafsi yake".

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Amebainisha wazi Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa imani kamili ya Muislamu yeyote haikamiliki mpaka apendeleee nduguye anachokipenda yeye, katika matendo mema, na aina mbalimbali za wema katika dini na dunia, na achukie kwake kinachochukiwa na nafsi yake, na ikiwa ataona kwa ndugu yake Muislamu kuna upungufu katika dini yake, basi ajitahidi kurekebisha, na akiona kuna jambo la kheri basi amtie moyo na amsaidie, na amnasihi katika dini yake au mambo ya dunia yake.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/66520>

